



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA
MAMLAKA YA UDHIBITI WA UNUNUZI WA UMMA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. FA.75/192/01/A/13

25 Juni, 2026

Kwa Taasisi Nunuzi Zote,
Zinazotumia Mfumo wa ERMS
Tanzania Bara

Yah: **WARAKA NA. 3 WA MWAKA 2025/2026 KUHUSU MATUMIZI YA MIFUMO YA
NeST NA ERMS KATIKA USIMAMIZI WA MIKATABA YA UNUNUZI WA UMMA
NA MALIPO**

Tafadhali rejeeni kichwa cha habari hapo juu pamoja na Kifungu cha 73 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 10 ya Mwaka 2023, kinachoelekeza kuwa shughuli zote za ununuzi, ugavi na uondoshaji wa mali zifanyike kupitia mfumo wa kielektroniki.

2. Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) inapenda kuzitaarifu Taasisi Nunuzi zote zinazotumia **Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali za Serikali (ERMS)** kuwa, kuanzia tarehe **1 Julai, 2026**, malipo yote yanayohusu mikataba ya ununuzi yanatakiwa kuanzishwa kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST) na kukamilishwa kupitia **ERMS**.

3. Kwa kuzingatia maelekezo hayo, Taasisi Nunuzi zote zinazotumia Mfumo wa ERMS zinatakiwa kuhakikisha kuwa zinatumia kikamilifu Moduli ya Usimamizi wa Mikataba iliyopo ndani ya NeST katika kusimamia utekelezaji wa mikataba, ikiwemo kupokea, kupitia na kushughulikia madai ya malipo yanayowasilishwa na wazabuni, washauri elekezi na watoa huduma.

4. Aidha, kuanzia tarehe **1 Julai, 2026**, haitaruhusiwa kufanya malipo ya mkataba wowote wa ununuzi ambao mchakato wake haukuanzishwa kupitia NeST. Hivyo, Taasisi Nunuzi zinapaswa kuhakikisha kuwa wazabuni, washauri elekezi na watoa huduma wanaelekezwa kuwasilisha madai yao ya malipo kupitia NeST kwa kuzingatia taratibu na masharti yaliyowekwa katika mfumo huo.

5. Taasisi Nunuzi zote zinaelekezwa kuzingatia na kutekeleza maelekezo haya ipasavyo ili kuhakikisha usimamizi wa mikataba na malipo ya ununuzi unafanyika kwa ufanisi, uwazi na kwa kuzingatia matakwa ya Sheria.

6. Nawatakia utekelezaji mwema.



Dennis K. Simba
MKURUGENZI MKUU